Dondoo za mkutano kati ya Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam (UWABA) na makau makuu ya traffic police

Tarehe 26 agosti 2009

Waliohudhuria
Komande Kombe - Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani
Inspector Mbunja - elimu
Inspector Avil Swai - elimu
Inspector Sarah Reuben - elimu
Inspector Teresa Kimaro
Inspector Nsokolo – mkuu wa elimu
Inspector Mpinya - engineer
Inspector Joseph Makabonga
Inspector Anthony Masanzu
Inspector Michael Deleli - takwimu
Inspector Mbuyule – kompyuta na takwimu
Inspector Bongwe – elimu
Inspector Emilian – takwimu na utafiti

Mejah Mbuya – mwenyekiti UWABA
Elaine Baker-Guni – katibu UWABA
Filbert Mbecha – mweka hazina UWABA
Sosthenes Amlima – Mjumbe wa kamati UWABA
Hussein Hamza – mwanachama UWABA
Hamadi Bwaja – mwanachama UWABA
Mohammed Samweli – mwanachama UWABA
Paulo Hatibu – mwanachama UWABA

Mejah na Elaine walieleza kwamba kuna matatizo ya service roads kwamba magari yanapaki kwenye service roads na kuziba njia na wapanda baisikeli na watembea kwa miguu wanalazimishwa kutumia barabara kubwa. Walionyesha photos za matatizo haya. TANROADS wameweka alama zinazoeleza ni marufuku kuegesha gari kwenye hifadhi ya barabara lakini bado matatizo yapo. Pia mwandishi wa habari wa gazeti ya Citizen, Junitha Makafu, aliwawa na pickup kwenye service road ya Sam Nujomba karibu na Mwenge tarehe 20 agosti wakati alitembea kwa miguu – kuna shida ya magari kuendesha haraka sana kwa hatari kwenye service roads. Pia magari yanatumia service roads ili kuruka foleni.

Mejah na Elaine pia walisema kwamba UWABA tunaendesha mradi wa kufundisha usalama wa baisikeli kwa wanafunzi wa shule na wapanda baisikeli wengine, kwa kutumia hela ya Wamba Memorial Fund ya $5,000. Tunatumia hela hii kuprint mwongozo, kununua helmets na reflective jackets kama zawadi, na kuwapa wanafunzi chakula wakati wa mafunzo. Tunapenda kuendelea kushirikiana na traffic police kuendesha mradi hii. Filbert alisema pole kwa Corporal Abuu ambaye alikuwa akihudhuria mafunzo yetu na aliyepata ajali.

Mejah alisema tunapenda kumwalika Komanda Kombe kuwa mgeni rasmi kwenye msafara wa baisikeli wa 2009 utatokea mwezi wa kumi na tulimpa karatasi ya maelezo ya msafara huu.

Mejah aliomba tuwe na walezi wa traffic police kuwasiliana nao kila mara.

Wanachama wengine wa UWABA walisema mara nyingine tunajaribu kupiga simu za traffic police zinazotangazwa lakini hazipatikani. Walisema mara nyingine gari inakaribia kugonga mpanda baisikeli lakini haigongi basi hakuna hatua traffic police wanachukua. Pia walipendekeza baadhi za ofisa za traffic police wasafiri na baisikeli na wataweza kufika sehemu ambazo hazifikishi na gari.

Inspector Bongwe alisema kwamba traffic police wanashirikiana kufundisha udereva Chuo cha Usafirishaji na VETA. Pia wanakagua magari. Alisema ni marufuku kuegesha gari kwenye service road. Inspector Deleli alitushauri UWABA tushirikiane na viongozi wa mitaa pia ili kuondoa matatizo haya. Pia alitushauri tutengeneze vipeperushi ili kueleza sheria. Inspector Mbuyale anafanya kazi ya Information Centre. Alisema kuna taratibu ya kuandika message kwenda kwa 0767750198 ili kutoa repoti ya matatizo na message inaingia moja kwa moja kwenye kompyuta. Inspector Mbunja alitushauri UWABA tuelimishe wapanda baisikeli kuweka kengele kwenye baisikeli. Inspector Emilian alisema kwamba idadi ya ofisa za traffic police hazitoshi basi wanategemea wananchi kutoa repoti kuhusu matatizo. Inspector Swai alisema traffic police wanatembelea kundi mbali mbali za watu ili kutoa elimu ya usalama barabarani. Inspector Reuben alitushauri tutengeneze sanaa na wimbo ili kuelimisha watu na Mejah alisema kwamba tayari tuna wimbo moja. Pia alitushuari tujaribu kupata namba ya registration ya gari inayovunja sheria au kugonga mtu kwa sababu ni ngumu kufuatalia bia namba hiyo. Pia alitushauria tuelimishe waendesha guta waendesha upande wa kushoto wa barabara na siyo kati kati ya barabara. Inspector Kimaro alitushauri tuelimishe wapanda baisikeli waendesha taratibu wakati wanapita sehemu penye watu wengi kama soko. Inspector Nsokolo alisema tuelimishe wapanda baisikeli watumie njia ya baisikeli kama ipo mfano kwenye Nyerere Road. Elaine alisema ni barabara chache zina alama ya kusema wapanda baisikeli watumie njia gani. Inspector Makabonga alitushauri tutumie kanuni za barabarani kwenye mafunzo yetu. Inspector Masanzu alitushauri tuelimishe wapanda baisikeli tushuke baisikeli wakati wa kuvuka kwenye zebra. Pia alitukaribisha kwenye wiki ya usalama barabarani mijni Mbeya. Inpsector Mpinya alitupongeza UWABA kwa ushirikiano wetu kwenye mkutano wa usalama barabarani hoteli ya Kempinski. Pia alitupongeza kwa kuwa na website nzuri. Alisema kwamba yeye anashirikiana na TANROADS kufanya road audit kuangalia usalama wa barabara zinazojengwa.

Komanda Kombe alisema walezi wetu watakuwa Inspector Avil Swai na Inspector Sarah Reuben, na UWABA tulishukuru. Komanda Kombe alitupa nakala ya Kanuni za barabara bure, ambayo kawaidia inauzwa. UWABA tulishukuru sana na tulisema tutatumia wakati wa mafunzo na kuweka ofisini ili wanachama wasome. Pia alitupa vipeperushi vinavyo namba za simu kupiga wakati kuna shida barabarani. Alieleza

kwamba magari wanaruhusu kutumia service road wakati wa dharua na pia kuingia kwenye plot, basi siyo njia na wapanda baisikeli na watembea kwa miguu pekee. Alisema afadhali barabara ziwe na njia maalum za wapanda baisikeli kama zipo Tabora. Alisema kuna matatizo ya miundombinu. Elaine alisema ni kweli na UWABA tunawasiliana sana na TANROADS, na TANROADS walituandikia barua kusema kwamba Kilwa road na Sam Nujoma road zitakuwa na njia maalum ya baisikeli lakini hawakutekeleza ahadi hii. Komanda Kombe alisema ni marufuku kuegesha gari kwenye service road na sheria ya barabara section 71a inasema hiyo. Alisema ni wazo mzuri kuwa na baadhi ya traffic police wanaosafiri na baisikeli. Aliomba UWABA tuwape traffic police nakala ya katiba yetu. Alishauri UWABA tuangalie nchi nzima na siyo Dar es Salaam tu. Elaine alieleza kwamba cheti cha usajili cha Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam ni cha Dar es Salaam tu lakini tutajaribu kusaidia wapanda baisikeli wa mikoa mengine kuanzisha vyama vya UWABA huko. Komanda Kombe alitupa takwimu kuhusu ajali za baisikeli. Alisema tutoe ripoti kwa simu kuhusu matatizo na kama tuwape photo za matatizo na wakitumia photo watatupa hela. Alisema ni muhimu wapanda baisikeli tuangalie nyuma kabla ya kupitia mtu, shimo n.k. Elaine aliomba traffic police watoe tangazo la kuelimisha sheria ya matumizi ya service roads. Komanda Kombe alisema tuandae draft ya tangazo na watapitia na kutoa. Alisema kila mtumiaji wa barabara na majibu. Wana mpango wakuanzisha mradi wa Road Marshalls ambao watakuwa waraia wanao elimu ya sheria ya barabara na uwezo wa kukamata watu wanaovunja sheria. Kuhusu mgeni rasmi kwenye msafara, alisema tumwandike barua ya kumwalika. Alisema pia ni koza kwa magari kutumia service road kuruka foleni kama hakuna dharua. Pia alitukaribisha kwenye wiki ya usalama barabarani mijni Mbeya – hawana fedha ya kulipa usafari wetu kuhudhuria lakini itakuwa nzuri tutafute fedha na kuhudhuria.

Mejah alishukuru sana Komanda Kombe na inspecta wa traffic police kwa mkutano mzuri na tutaendelea kushirikiana. Komanda Kombe alisema Mejah na wanachama wengine wamefanya kazi nzuri kuanzisha na kuendesha chama cha UWABA kwa kujitolea.